# »Kuchagua eneo la kufugia ya nyuki«

Ufugaji wa nyuki ni biashara yenye faida, kwani asali hutoa faida nyingi za kiafya. Ni muhimu kuwa na ujuzi juu ya uchaguzi wa eneo la kufugia nyuki, na mbinu za usimamizi wa nyuki kabla ya kuanzisha mradi.

Hata hivyo, usianzishe maeneo ya kufugia nyuki katika maeneo yanayonyunyiziwa na viuatilifu, viwanda vya sukari na viwanda vingine kwani nyuki hupata protini au dutu tamu kutoka kwa vyanzo hivyo.

## Miongozo ya uchaguzi wa eneo

Daima weka mizinga ya nyuki katika katika maeneo ambayo yanaweza kufikiwa kwa urahisi. Vile vile, chagua maeneo yenye aina za mimea ambayo huchanua maua mengi ili kuwapa nyuki utomvu na chavua ya kutosha kwa ajili ya kutengeneza asali.

Chagua eneo lenye vyanzo vya maji bora kwa vile kila kundi la nyuki linaweza kutumia hadi lita 4 za maji kwa siku wakati wa hali ya hewa ni joto. Maeneo ya kufugia nyuki yanapaswa kuwa karibu na nyumbani ili kupunguza gharama za usafiri na usimamizi.

Chagua maeneo tambarare ili kurahisisha shughuli za usimamizi. Pia maeneo yanapaswa kuwa na kivuli. Hata hivyo, epuka maeneo yenye mafuriko, moto, wizi, na uharibifu, kwani haya yanaweza kupunguza uzalishaji wa asali.

## Usimamizi wa eneo la kufugia nyuki

Chunguza eneo kila mara, dhibiti wadudu waharibifu. Weka mizinga ya nyuki juu ya ardhi. Fanya uchunguzi wa mara kwa mara ili kuona chavua iliyohifadhiwa.

Pia weka mizinga ya nyuki mbali na binadamu, zingatia idadi ya makundi ya nyuki, na viingilio vya mizinga visielekee moja kwa moja kwenye mwanga wa jua kwa vile huku kunaweza kupunguza uzalishaji wa asali. Kagua eneo kwa uangalifu kuhakikisha kwamba mimea na miti haina nekta na wadudu wa kuchavusha.